

# SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



## Hadithi Angani



"Kioo, kioo katika ukuta, je ni nani amepauka zaidi?" Iliuliza nyota inang'aayo huku ikingalia taswira yake iliyoakisiwa katika punje za vumbi angani. Ilistaajabu sana iliposikia jibu. "Haya ni mawingu ya vumbi"

Sawa, ni kueli nyota haziwezi kuongea, lakini haya mawingu ya vumbi ni mazuri zaidi kuliko nyota zinazoyamulika. Yanaitwa nebula akisi (reflection nebulae) kwa sababu yana akisi mwanga kutoka katika nyota zilizo karibu nayo na nebulae ni neno la kilatini linalomaanisha 'mawingu'

Nyota iliyoakisiwa imeonyeshwa katika rangi ya bluu na nyeupe katika picha. Vumbi pia hutengeneza mwanga wake wenyewe, mwanga ambao umeonyeshwa kwa rangi ya chungwa katika picha. Sehemu hizi zenye rangi ya chungwa zinaonyesha sehemu mavumbi yalipolundikana.

Macho yetu hayawezi kuona hata kidogo mwanga unaotoka katika vumbi, lakini darubini maalum iitwayo APEX inaweza kuona. Bila APEX, wanaanga badala ya kuona milundikano ya mavumbi wasingeona kitu chochote - pangkuwa na giza nene, ambalo lingezuia kutambua chochote kilichopo.

Lakini ni muhimu kwa wanaanga kuweza kutazama eneo hili, kwani nyota mpya zinazaliwa katika mawingu haya ya vumbi na gesi.

### COOL FACT

Darubini ya APEX inapatikana katika jangwa lililopo Marekani ya Kusini ambalo lipo mita 5100 juu ya usawa wa bahari!



More information about EU-UNAWE Space Scoop: [www.eu-unawe.org/kids/](http://www.eu-unawe.org/kids/)